JOURNEYS of SOLUTIONS

# Suluhisho la Safari (JOS) – Mpango wa udhamini wa mtoto
## Maswali yanayoulizwa mara kwa mara na mfuko wa Kesho (MASWALI)
## "Kesho Fund"

1. **Mfuko wa Kesho – Kesho Fund – ni nini?**

   Kesho Fund (Mfuko wa Kesho) ni sehemu ya programu ya msaada wa watoto wa ufumbuzi (CSP). Mfuko wa Kesho uliundwa mnamo 2017 kusaidia juhudi za elimu ya juu, yaani elimu zaidi ya kidato cha IV, na mwisho wa mradi huu ni mwaka 2027, pamoja na CSP. Tunatarajia kufunga CSP wakati wanafunzi wetu wa mwisho wanamaliza elimu yao ya juu, ambayo inaweza kuwa miaka kumi na minane tangu kuanzishwa kwa CSP. Tangu 2017, jumla ya michango kwa CSP na ile iliyoangaziwa "Mfuko wa Kesho" imewasaidia wanafunzi wanaohitimu na wanaotamani kuendelea na elimu ya juu au kupewa ruzuku ya wakati mmoja kwa ajili ya kusaidia kuanzisha biashara. Mara tu mwanafunzi anapohitimu kidato cha IV, lazima awasilishe ombi kwa Mfuko wa Kesho la kuendelea na elimu au ombi la ufadhili wa biashara, hata kama ana udhamini wa mtu binafsi.

2. **Mwanafunzi anafuzu vipi kupata msaada wa Mfuko wa Kesho?**

   Msaada wa Mfuko wa Kesho unapewa kipaumbele kwa wanafunzi waliojiunga na mpango wa msaada wa mtoto wa JOS (CSP) ambao wanafanya vizuri katika masomo yao na wamekuwa wakiendeleza matokeo mazuri ya taaluma na taarifa zuri kitabia.
   Kwa upande wa wanafunzi walio nje ya CSP ambao wanavutiwa na msaada wa Mfuko wa Kesho, JOS inakubali maombi katika kipindi cha Februari kila mwaka. Maombi yaliyo kamili pekee ndio yatazingatiwa na lazima yawasilishwe angalau miezi 6 kabla ya kozi unayotaka kusoma na/au kutekeleza azma ya biashara unayokusudia kufanya. Ruzuku hii hutolewa kama msaada kwa mara moja tu.

3. **Ni miaka mingapi Msaada wa Mfuko wa Kesho utakuwepo kumsaidia mwanafunzi?**

   Hii itatofautiana kulingana na hali ya mwanafunzi; tazama mifano hapa chini.
   Katika hali yoyote, utendaji wa kitaaluma wa mwanafunzi na tabia zitatathminiwa katika kila kipindi cha miezi sita ili kuhakikisha kuwa msaada utaendelea. Hata hivyo, ombi la ruzuku la kila mwaka katika Mfuko wa Kesho litahitajika.

   - Kwa wahitimu wa kidato cha IV wa daraja la 1 au 2, muda wa **hadi miaka mitano** utazingatiwa.
   - Kwa wahitimu wa kidato cha IV wa daraja la 3 au 4 au mwanafunzi wasio na cheti cha kidato cha IV, muda wa **hadi miaka mitatu** utazingatiwa.

4. **Je, Wanafunzi wa CSP waliojiunga kwa sasa na shule ya sekondari hupewa msaada wa Mfuko wa Kesho wakati wa kuhitimu kidato cha IV?**

   Inategemea! Msaada wa Mfuko wa Kesho haupaswi kudhaniwa kuwa ni kwa ajili ya wahitimu wote wa kidato cha IV wa CSP. Badala yake, ni kama ilivyoelezwa katika kipengele (tazama # 3) hapo juu kuwa ni wale wenye matokeo ya daraja la 1 na 2 ambao wamefuzu kuingia kidato cha V watastahili kupatiwa moja kwa moja msaada wa Mfuko wa Kesho wa kufikia hadi Tsh 5,798,000/- kwa mwaka kwa kidato cha V. Na kwa masomo ya kidato cha VI, wanafunzi lazima watimize sharti la maendeleo mazuri kitaaluma, kama ilivyofafanuliwa hapo chini katika vipengele (tazama #15, #16, na #17).

   Kwa wahitimu wa kidato cha IV ambao wamepata matokeo kwa daraja la tatu **III** au daraja la nne **IV** ambao wanatarajia kuendelea na masomo lazima wapeleke maombi kwa Mfuko wa Kesho angalau miezi miwili kabla ya kozi inayofuata ya masomo kuanza. Matokeo mazuri ya kitaaluma na kitabia kwa mwanafuzi itazingatiwa kwa kila mwaka kabla ya kufadhiliwa tena.

5. **Je, ni kiasi gani cha fedha za msaada kwa mwanafunzi kinapatikana kupitia Mfuko wa Kesho?**
   Kiasi cha fedha kinategemea na kiasi kilichoombwa kwa Mfuko wa Kesho; tazama hapa chini kwa mifano kadhaa.
   - **Mafunzo ya elimu ya juu|** Baada ya kuwasilisha "ombi kwa Mfuko wa Kesho - kwa ajili ya kujiendeleza kielimu" na kupitishwa, wanafunzi watastahili kupata hadi kiasi cha Tsh 5,798,000/-kwa mwaka kwa kozi za masomo ya juu kama kidato cha V na kidato cha VI, cheti au kozi ya stashahada. Kiasi hiki kinajumuisha gharama za kila mwezi za kuishi wakati wote wa mpango huu na fursa za ziada za kitaaluma pamoja na gharama za makazi kulingana na mihula ya shule au chuo.
   - **Mpango wa mafunzo ya uanzaji wa kazi "Jobortunity" |** Baada ya kuwasilisha "ombi kwa Mfuko wa Kesho - kwa ajili ya gharama ya kujiendeleza na mafunzo" na kufanikiwa kumaliza mchakato wa usajili wanafunzi watastahili kupata hadi kiasi cha Tsh 2,783,000/- kukamilisha mpango wa kazi. Kiasi hiki kinaweza kujumuisha gharama za kila mwezi za kuishi wakati wote wa mpango huu. **KUMBUKA:** kiasi cha Tsh 115,000/- watapewa wanafunzi wanaostahili ili waweze kukamilisha mchakato wa usajili.
   - **Kozi ya Udereva** | Baada ya kuwasilisha "ombi kwa Mfuko wa Kesho kwa ajili ya kuendelea na masomo" na kupitishwa mwanafunzi atakuwa anastahili kupewa hadi kiasi cha Tsh 692,000/- kwa ajili ya gharama za uandikishwaji, usafiri, malazi na ada ya leseni.
   - **Kozi ya Lugha** | Baada ya kuwasilisha "ombi kwa Mfuko wa Kesho kwa ajili ya kuendelea na masomo" na kupitishwa mwanafunzi atakuwa anastahili kupewa hadi kiasi cha Tsh 692,000/- kwa ajili ya garama za uandikishwaji, usafiri, na malazi.
   - **Ruzuku ya Biashara**| Baada ya kuwasilisha "ombi kwa Mfuko wa Kesho maombi ya Biashara" pamoja na mchanganuo kamili wa mradi, mwanafunzi anastahili kupata ruzuku ya wakati mmoja hadi kiasi cha Tsh 1,150,000/-.

6. **Ikiwa wanafunzi wataamua kuacha masomo kabla ya kipindi cha ufadhili wa miaka 3 au 5, Je, wanastahili msaada wa Mfuko wa Kesho katika siku zijazo?**
   Inategemea! Wanafunzi wanastahili kupata fedha ndani ya vipindi vyao husika vya ufadhili tu. mfano miaka 3 au 5 kutoka kipindi walipoanza kozi yao ya kwanza ya elimu ya juu.

   Wanafunzi lazima wawasilishe maombi katika Mfuko wa Kesho ili waweze kupata fedha. Maombi haya yafanyike miezi 2 kabla ya tarehe ya kuanza mhula mpya wa masomo. Kwa wanafunzi walio na wadhamini binafsi Ikiwa fedha hazijaombewa au hazijapokelewa ndani ya kipindi cha dirisha la ufadhili, wadhamini watajulishwa na fedha zinaweza kuelekezwa kumsaidia mwanafunzi mwingine.

7. **Je, Wanafunzi walio na utendaji bora kitaaluma na tabia wataweza kupata msaada wa Mfuko wa Kesho zaidi ya kipindi cha miaka 3- au 5- iliyoainishwa hapo juu?**
   Inategemea! Kwa hali ya kipekee, wanafunzi wanaweza kustahili kupata fedha za ziada za masomo zaidi ya kipindi cha muda wa miaka 3 au 5. Maamuzi yatazingatiwa ikiwa maombi hayo yamewasilishwa miezi sita kabla ya mwisho wa kozi ya masomo ya mwanafunzi. Wanafunzi lazima wapeleke maombi yaliyokamilika kwa Mfuko wa Kesho.

8. **Ni nini hufanyika mara mwanafunzi atakapokamilisha kipindi chake cha miaka 3 au 5 ya ufadhili?**
   Wanafunzi ambao wanamaliza kwa ukamilifu elimu ya juu watastahili kupatiwa ruzuku ya mpito kwa wakati mmoja hadi kiasi cha Tsh 1,150,000/-. JOS itasaidiana na wanafunzi kubaini fursa ya ajira inayokubalika, usaidizi unaohitajika na msaada mwingineo. Mwanafunzi lazima apeleke maombi kwa Mfuko wa Kesho "ombi kwa Mfuko wa Kesho maombi ya Biashara."

9. **Je, itakuwaje kama gharama ya mafunzo/matumizi ikizidi kiasi alichopewa mwanafunzi?**
Ikitokea gharama zinazidi kiasi alichopewa (tazama # 5) mlezi au mwanafunzi atawajibika kulipa tofauti hiyo. Mwanafunzi atakiri kuwa kushindwa kulipa kunaweza kusababisha mwanafunzi kurudishwa nyumbani kutokana na hali ya kukosa fedha za shule, au mwanafunzi hatakuwa na gharama za mahitaji ya kila mwezi kama vile kodi, chakula na mahitaji muhimu kama wanavyopatiwa katika kipindi cha kawaida, JOS itafanya makubalino ya maandishi kwa kadri inavyowezekana kuhusiana na jambo hilo. Na vile vile JOS itamjulisha mwanafunzi, au Familia miezi miwili kabla ya fedha kwisha au kumalizika ili waweze kufanya mpango wa malipo.

10. **Je, Wanafunzi wanapatiwa simu au kompyuta mpakato kwa ajili ya matumizi wakati wa mihula ya masomo?**
Mara nyingi na haswa kwa wanafuzi wa chuo hupatiwa. Kutokana na kwamba kujifunza kwa njia ya mtandao ni muhimu haswa kwa wanafunzi wa ngazi ya chuo. Wanafunzi wa chuo hupatiwa simu na kompyuta mpakato kwa matumizi yake chuoni. Vifaa hivi hupewa mapema kabla hawajaanza mhula wa mwanzo wa masomo. Wanafunzi wanapaswa kutunza vifaa hivyo kwani vikiharibika gharama za matengenezo zitatolewa kutoka katika ruzuku yake. Kadi za simu zitakuwepo pamoja na kiasi kidogo muda wa maongezi ili kuhakikisha kuwa shughuli za kujifunza kwa mwanafunzi hazitathiriwa. Mwanafunzi akipoteza simu au kompyuta mpakato atoe taarifa haraka kwa JOS. Hakuna uhakikisho kuwa kifaa kingine kitatolewa baada ya kupoteza au kuharibu ya awali. Wanafunzi wakisimamishwa masomo au wakaondolewa katika mfuko wa msaada wa kesho kompyuta mpakato pamoja na simu ni lazima zirudishwe JOS.

Kwa kuwa shule nyingi za sekondari haziruhusu matumizi ya simu wanafunzi wa sekondari watapatiwa simu ndogo ambazo zitatunzwa na mwalimu au uongozi wa shule wakati wa kipindi cha katikati ya muhula wa masomo. Hii itaamuliwa kulingana na hali ya mazingira yatakavyokuwa. Kama shule hairuhusu matumizi ya simu kwa wanafunzi na mwanafunzi akakiuka sheria hiyo na simu kunyanganywa JOS haitanunua simu nyingine mbadala. Ikumbukwe kuwa Kompyuta mpakato hazitatolewa kwa mwanafunzi wa sekondari.

11. **Je, JOS inatoa msaada katika kipindi cha katikati ya muhula wa masomo?**
Ndiyo kihistoria JOS hutoa ruzuku kwa ajili ya mafunzo, chumba pamoja na kozi za ziada katika kipindi cha katikati ya muhula, hususani kwa wanafunzi wanaosubiri kujiunga na elimu ya juu (inaweza ikawa hadi miezi 9), JOS inashirikiana na wanafunzi ili kuhakikisha kuwa wanajiunga na mafunzo mbalimbali na au katika nafasi za kujitolea.

Kwa wanafunzi wenye umri wa zaidi ya miaka 18 (wenye matokeo mazuri ya kitaaluma na nidhamu) ambao watakuwa wanahesabiwa kuwa ni watu wazima kisheria hawawezi tena kuruhusiwa kuishi Shalom Orphanage,[1] Mfuko wa Kesho utawapatia gharama za makazi na nyumba katika kipindi cha mihula ya masomo ili waweze kuendeleza ndoto zao za kielimu katika maeneo yaliyo karibu kabisa na taasisi wanazosomea.

Pia watapatiwa kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya gharama za usafiri. Malipo yatafanyika moja kwa moja kwenye nyumba ya wageni au kituo anachokaa (kwa makaazi yaliyopo pembezoni) lakini kutegemea na mazingira wanafunzi wanaweza kupokea malipo haya wenyewe. Katika mazingira ambayo wanafunzi watapokea fedha wenyewe basi risiti za malipo zote zihifadhiwe na kisha kukabidhiwa kwa JOS.

JOS haitarajii kuwa itafanya malezi kwa wanafunzi wenye zaidi ya miaka 18, japo itasaidia wanafunzi kubaini washauri na msaada mwingine utakavyohitajika. Na iwapo mwanafunzi amechagua kuishi na mlezi au mwana familia katika vipindi vya likizo, JOS inaweza ikatoa kiwango kidogo cha fedha ili kusaidia huduma ya chakula na mahitaji mengine kwa familia hiyo.

---

[1] Kwa mujibu wa kipengele cha 138 cha sheria ya watoto 2009, "wale ambao wana umri wa zaidi ya miaka 18, hawaruhusiwi kuishi katika nyumba ya kulelea watoto au kituo cha kulelea watoto yatima pamoja na watoto wengine walio na umri chini ya miaka 18.

12. **Je, ni kiwango gani cha jitihada kinahitajika kutoka kwa mwanafunzi iwapo anaishi kwa kujitegemea au anaishi na mlezi?**
Kiwango fulani cha jitihada kinahitajika kutoka kwa mwanafunzi au mlezi au familia. Hii inaweza kuhusisha lakini haizuiliwi kuzidi haya yatanjwa hapo chini: makazi wakati wa kusoma au wakati wa likizo, kupatiwa fedha za safari kwenda/kurudi shuleni, kupatiwa simu na vocha kwa mwanafunzi, kupatiwa fedha ya matumizi, kununua vitu vya shule na kama ilivyo kawaida. JOS itamwarifu mwanafunzi, mlezi na familia miezi miwili kabla ya fedha kumalizika ili waweze kufanya maandalizi ya malipo.

13. **Ni, kwa namna gani jitihada za Mfadhili zinazingatiwa?**
Tunaona fahari kubwa kwa wafadhili wetu mmoja mmoja kuweza kushirikiana na wanafunzi wakati wakiwa wanaogelea kwenye uelekeo wao wa kielimu.

Ikitokea kwamba mfadhili binafsi ameamua kujiondoa katika kusaidia na mwanafunzi amekuwa na historia nzuri ya maendeleo ya kitaaluma na kinidhamu katika mitihani yake ya muhula na mwaka, mwanafunzi atakuwa amefuzu kuingia katika kusaidiwa na Mfuko wa Kesho kwa kuwasilisha maombi stahiki. (Ruzuku ya biashara au kuendelea na masomo).

Iwapo mfadhili ameamua kujiondoa na mwanafunzi hana matokeo mazuri ya kitaaluma au ya kinidhamu katika muhula au mwisho wa mwaka, hapatakuwa na ruzuku yoyote itakayotolewa tena kama ambavyo imeainishwa hapo chini (tazama #15, #16, #17).

14. **Je, ni sheria zipi zinasimamia wanufaika wa Mfuko wa Kesho kuhusiana na mawasiliano na wafadhili?**
Kutokana na mazingira ya kazi zetu ya kufanya na jamii inayoishi katika mazingira hatarishi/ jamii isiyofikiwa ya Tanzania, mawasiliano ya moja kwa moja kati ya wafadhili na wanafunzi hayaruhisiwi katika kipindi chote cha ufadhili. Mawasiliano yote lazima yapitie JOS; hii itahusisha mawasiliano kwa barua, picha, video nk.

Hii haitokani na kukosekana kwa uaminifu kati ya wafadhili au wanafunzi, badala yake itasaidia kuepusha kuzalisha matarajio yasiyo ya lazima ya mahusiano kati ya mfadhili na mwanafuzi kwa pande zote ambayo yanaweza kusababisha matokeo mabaya kwa wanafunzi.
Hata baada ya kumaliza mchakato wa kielimu na pia kuingia katika maisha ya kujitegemea JOS itabaki kuwa kiungo kati ya mwanafunzi na mfadhili au wafadhili.

15. **Je, wanafunzi wanapimwaje kitaaluma?**
Maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi hupimwa moja kwa moja na taasisi aliyopo, au mlezi au familia katika kipindi cha miezi sita (kila muhula).
    - **Wanafunzi wa kidato cha V na VI |** Wanafunzi ni sharti wawe na daraja A kwenye mitihani mingi pamoja na daraja B au GPA 2.5 au zaidi kwa kila mwaka ili aweze kupewa nafasi ya kuendelea na mwaka mwingine wa ufadhili.
    - **Wanafunzi wanaosomea Astashahada au Stashahada |** Wanafunzi ni sharti wawe na daraja A au B /au GPA 2.5 au zaidi kwa kila mwaka ili aweze kupewa nafasi ya kuendelea na mwaka mwingine wa ufadhili.
    - **Wanafunzi wanaosoma vyuo vya ufundi** | Wanafunzi ni sharti wawe na daraja au wastani wa B au zaidi kwa kila mwaka ili waweze kupewa nafasi ya kuendelea na mwaka mwingine wa ufadhili. Katika mazingira ambayo madaraja au GPA haizingatiwi katika matokeo, taarifa au mapendekezo au maoni ya maadishi kutoka kwa utawala au kiongozi wa ngazi ya juu wa taasisi itakubalika.

16. **Je, wanafunzi wanapimwaje kitabia?**
Kama nyongeza katika kuzingatia kiwango cha juu cha matokeo kitaaluma, wanafunzi wanapaswa kuzingatia kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika kipindi chao chote cha ufadhili. Ikiwa ni pamoja na kuhudhuria kikamilifu vipindi vyote darasani, nidhamu ya fedha n.k. Mazingira ya sekondari, haswa kwa wale waliochagua kuishi bweni, wanaonekana kuwa na sheria ngumu zaidi ukilinganisha na taasisi za elimu ya juu ambayo wanafunzi wana uhuru zaidi juu ya ratiba zao, wanaweza kuishi nje ya chuo n.k kwa kadiri wanafunzi wanavyozoea uhuru wao mpya, tunategemea kuona wanaendelea kuwa na maendeleo mazuri kitaaluma na kinidhamu (tazama #17 na #19).

17. **Ikiwa maendeleo ya kitaaluma na kitabia kwa mwanafunzi yatakuwa sio mazuri, Je wanapewa muda wa ziada wa matazamio ili waweze kujirekebisha?**
Ndio! Tunawapa wanafunzi fursa ya kujirekebisha kadiri iwezekanavyo ili wapate maendeleo mazuri.

Kwa upande wa maendeleo ya kitaaluma (tazama #15): katika matokeo ya mwisho wa muhula wa kwanza mwanafunzi kama hakupata daraja kulingana na kiwango kinachotarajiwa, atapewa kipindi kingine cha miezi sita zaidi kurekebisha matokeo yake. Mwisho wa mwaka kama hakuweza kufanya vizuri tena mwanafunzi ataondolewa katika mpango na msaada kusitishwa. Hakutakuwa na ulazima katika maamuzi ya kupewa ama kutopewa ruzuku ya mkupuo mmoja.

Katika tukio la kosa la kwanza la kinidhamu (tazama #19), mwanafunzi atapewa onyo la mdomo na maandishi mara moja na miezi miwili itatolewa kwa ajili ya kurekebisha tabia vinginevyo msaada utasitishwa. Viongozi wa shule watasaidia katika kuhakikisha kuwa tabia imerekebika. Mwanafunzi atapaswa pia kuomba msamaha kwa maandishi kwa mtu au ofisi aliyoikosea. huku akifafanua sababu za utovu wa nidhamu.

Katika tukio la kosa la pili la kinidhamu mwanafunzi ataondolewa katika mpango wa ufadhili katika kipindi cha mwezi mmoja. Hakutakuwa na ulazima katika maamuzi ya kupewa ama kutopewa ruzuku ya mkupuo mmoja.

18. **Ikiwa mwanafunzi ameondolewa katika mpango wa ufadhili wa JOS kutokana na matatizo ya kinidhamu atakuwa amepigwa marufuku kuingia katika ufadhili mwingine katika kipindi cha baadaye?**
Kwa sehemu kubwa ndiyo, isipokuwa kwa wanafunzi wa kike ambao wamepata ujauzito wakati wa masomo. Kama mwanafunzi hakuweza kumaliza masomo yake kutokana na sheria za taasisi anaweza kupatiwa ruzuku iliyobaki kwa kuwasilisha fomu ya maombi ya Mfuko wa Kesho. Akipatiwa ruzuku hiyo anaweza kushauriwa kugharamia elimu yake katika taasisi nyingine au aipeleke katika biashara (tazama #19 kwa ajili ya maelekezo ya kina juu ya mimba).

19. **Je, ni mifano gani huonesha utovu wa nidhamu?**
    - **Matumizi mabaya ya Ada ya shule/Mpango |** mwanafunzi anapotumia vibaya ada aliyopewa kwa ajilil ya masomo, atalazimika kurudisha kiasi chote kwa JOS ndani ya kipindi cha miezi miwili ili kuahakikisha kuwa ataendelea na ufadhili na pia ataonywa kwa mdomo na kwa maandishi.
        - Mwanafunzi anapaswa kuandika barua inayoelezea matumizi mabaya ya fedha na awasilishe kwa JOS na shule ndani ya kipindi cha wiki moja.
        - Ikiwa mwanafunzi atarudisha fedha ndani ya kipindi hiki, ataweza kuendelea kusoma na malipo yoyote ya shule yaliyobaki kwa mwaka huo yatalipwa na JOS.
        - Ikiwa mwanafunzi hataweza kulipa pesa hizo kwa muda wa miezi miwili, kiasi hicho cha fedha kitaondolewa kutoka katika ruzuku ya kipindi kijacho cha ada ya mwaka huo wa masomo. Hii ina maanisha deni lolote linalodaiwa na shule au taasisi litakuwa linamhusu mwanafunzi huyo au familia na sio JOS. Mwanafunzi anafahamishwa kuwa kushindwa kulipa deni hilo kwa JOS au shule au taasisi, inaweza ikasababisha mwanafunzi kurudishwa nyumbani hadi deni hilo litakapolipwa lote.
        - Iwapo malipo hayajafanywa kwa JOS ndani ya kipindi cha miezi sita, msaada wote utasitishwa na mwanafunzi hataweza tena kuingia katika mpango wowote ujao wa ufadhili au ruzuku ya mkupuo mmoja.

- **Gharama za kuishi |** ikiwa mwanafunzi atatatumia vibaya fedha zilizokusudiwa kumsaidia kukudhi mahitaji yake ya mwezi mfano inaweza kuwa kuwasilisha bajeti inayozidi kwa ajili ya mahitaji ya mwezi au kupoteza vifaa mara kwa mara, kuwa mzembe katika matumizi ya fedha za kujikimu, atahitajika kulipa fedha zote kwa JOS ndani ya kipindi cha miezi miwili.
    - Mwanafunzi atalazimika kuandika barua na kueleza jinsi matumizi mabaya ya fedha zilivyotokea na kukabidhi kwa JOS au shule au taasisi husika ndani ya kipindi cha juma moja.
    - Mwanafunzi anaweza akaamua kiasi cha fedha cha kuondolewa katika fungu lake la fedha za matumizi au atalazimika kulipa taslimu ndani ya kipindi cha miezi miwili, kama mwanafunzi ataweza kulipa fedha ndani ya kipindi hiki, atakuwa anafuzu kupokea ruzuku ya matumizi kwa kiasi kili kile anachopokea kawaida.
    - Ikiwa mwanafunzi hakuweza kulipa ruzuku hiyo ndani ya kipindi cha miezi miwili, familia yake au mlezi atahusika na kulipa deni hilo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa mwanafunzi ataendelea kupatiwa ruzuku za JOS kwa ajili ya gharama za maisha. Kushindwa kulipa fedha za JOS kutasababisha kutopatiwa tena ruzuku ya matumizi hadi deni hilo lilipwe lote.
    - Iwapo malipo hayajafanyika kwa JOS ndani ya kipindi cha miezi sita, malipo yote yatasitishwa na mwanafunzi hataweza kufuzu kupokea msaada mwingine wa ruzuku ya mkupuo mmoja.
    - Iwapo mwanafunzi ataibiwa kifaa, atapaswa kutoa taarifa haraka kwa JOS na ikiwa sababu zitaeleweka, JOS inaweza kutoa fedha za kununua kifaa hicho ndani ya kipindi cha mwezi huo. Lakini ikiwa kifaa hicho kiliibiwa kwa sababu ya uzembe mfano sanduku kuachwa wazi au utunzaji mbaya wa vifaa, JOS haitatoa fedha za kununua tena vifaa hivyo kwa mwezi huo. Mlezi wa mwanafunzi au familia yake, hawana budi mumpatia kifaa hicho kilichopotea.
    - Katika hali ya dharura ambayo itahitaji fedha ambazo mwanafunzi hana, gharama zilizoidhinishwa pekee ndiizo zitatolewa. Mwanafunzi ni sharti awasiliane haraka na JOS kuelezea uhitaji. Iwapo mwanafunzi hakuwasiliana na JOS na badala yake akaamua kukopa fedha kwa mtu basi JOS haitahusika na malipo ya deni hilo.

- **Taarifa ya mwanafunzi isiyo nzuri kutoka shuleni au Shirika au JOS |** Ifuatayo ni mifano**:**
    - Uharibifu na/ au wizi kutoka kwa wanafunzi wengine au mali ya shule
    - Kufanya Udanganyifu kwa wasimamizi wa shule, JOS au familia
    - Kushuka kwa kiwango cha mahudhurio au kutokuwepo shuleni, kukwepa vipindi, kutojitunza mwenyewe (kutokutoa taarifa au kutokutoa taarifa sahihi kuhusu afya) na mengine.
      **KUMBUKA:** Wanafunzi wanapatiwa ruzuku kwa ajili ya huduma stahiki za afya kwa hiyo ni lazima wajitunze kikamilifu, watumie dawa kadri ya maelekezo ya tabibu, katika mazingira ya kushindwa kuhudhuria shule kutokana na sababu za kiafya, JOS itawasiliana na shule na hospitali kuhusu uwezekano wa mwanafunzi huyo kuendelea na masomo bila ya mwanafunzi huyo kurudia mwaka.

- **Mimba|** Kwa kuwa JOS hutoa msaada wa masuala ya kielimu, fedha za ufadhili zipo kwa ajili ya masuala ya kielimu pekee. Ikitokea mwanafunzi aliyefadhiliwa akapata ujauzito au kumpatia mimba mtu yeyote, msaada wao unaweza kusitishwa ndani ya kipindi cha mwisho wa mwaka huo. Iwapo mwanafunzi ana mfadhili binafsi, mfadhili huyo ataelezwa. Hata hivyo maamuzi ya mwisho kuhusu ustawi wa mwanafunzi uko mikononi mwa mlezi au familia au mwanafunzi mwenyewe au na JOS. Ikitokea mwanafunzi amefukuzwa na mlezi au kuondoka utunzaji wa walezi, JOS haiwezi kuwa mlezi wa mwanfunzi huyo au mtoto wake.
  **KUMBUKA:** Sera hii haitumiki kwa wanafunzi wa kike ambao wanaweza kuwa walibakwa na kisha wakapata ujauzito. JOS itashirikiana pamoja na walezi katika mambo haya pia na inaweza kushauriana na taasisi za afya kwa msaada na ushauri na tiba. Katika hali ambayo mwanafunzi wa kiume atahusika katika tendo la ubakaji bila kujali kama aliyebakwa atapata ujauzito au la, huyo mwanafuzi wa kiume atasitishiwa ufadhili.
    - **MWANAFUNZI WA KIKE:** Ikiwa ada ya shule haijalipwa kwa mwaka na kuna fedha zilizobaki katika akaunti yake, JOS atawasiliana na uongozi wa shule hiyo kuona kama mwanafunzi anaweza kuendelea na masomo kabla hajafanya utaratibu wa malipo ya ada ya muhula mwingine au gharama za maitaji mengine.
        - Ikiwa taasisi anayosoma itamruhusu kuendelea na usajili wake basi ufadhili wa JOS utaendelea ifikapo mwisho wa muhula wa masomo.
        - Ikiwa mwanafunzi amefukuzwa shule kwa sababu taasisi ya elimu hairuhusu wasichana wajauzito kusoma, JOS itazingatia mwendelezo wa malipo ya ruzuku iliyobaki na kuitoa kwa mwanafunzi huyo mara moja pale tu atakapopeleka maombi na yakakubalika kama maombi ya ruzuku ya Mfuko wa Kesho.
    - **MWANAFUNZI WA KIKE:** Ikiwa ada ya shule tayari imelipwa kwa mwaka mwaka mzima na kuna fedha zilizobaki katika akaunti ya mwanafunzi, JOS itatoa gharama zinazohusiana na maisha ya kawaida wakati wa kusoma (hadi Tsh100,000/- kwa mwezi kulingana na kiasi kilichopo, kwa ajili ya miezi iliyobaki ya masomo ili mwanafunzi aweze kumaliza kiwango chake cha elimu na kutunukiwa cheti kulingana na kiwango cha elimu aliyosomea.
    - **MWANAFUNZI WA KIKE:** Ikiwa kuna kiwango cha fedha kilichobaki katika akaunti ya mwanafunzi, JOS itatoa kiasi cha ada ya matibabu na kiliniki wakati wa ujauzitio (hadi Tsh 100,000/-) na gharama za kujifungua katika hospitali ya FAME (hadi Tsh 150,000/-). Mwanafunzi atajigharamia mwenyewe usafiri kwenda FAME na mahitaji mengine yatakazojitokeza wakati wa kujifungua.
    - **MWANAFUNZI WA KIUME:** Ikiwa mwanafunzi aliyefadhiliwa atampa mtu yeyote ujauzito, ruzuku yake ya kielimu itaishia mwisho wa mwaka huo wa kielimu. Kwa maana inadhaniwa kuwa msaada wake kwa mama na mtoto utahitajika kupitia yeye kufanya kazi yakujipatia kipato.
    - **MWANAFUNZI WA KIKE/KIUME:** Mwanafunzi aliyefadhiliwa atapewa kipindi cha mwaka mmoja (kutoka wakati ruzuku yao imesitishwa) kuwasilisha maombi katika Mfuko wa Kesho kuomba ruzuku ya mkupuo mmoja, labda kwa ajili ya kujiendeleza kielimu au ruzuku ya biashara. Hakuna ulazima wa maamuzi ya kutolewa kwa ruzuku hii.

- **Shughuli za uhalifu/Kushitakiwa |** Kwa sehemu fulani ikitokea mwanafunzi anatuhumiwa kwa makosa ya jinai au kukamatwa na vyombo vya dola, Msaada wa Mfuko wa Kesho utasitishwa hadi mwanafunzi itakapothibitishwa kwamba hana hatia. Iwapo itathibitika kuwa ameshiriki jinai, wafadhili watajulishwa na ruzuku itaelekezwa kwa mwanafunzi mwingine.

- **Fursa nyingine mahususi anayopewa mwanafunzi aliyepoteza fursa ya kwanza|** mwanafunzi anapokuwa amewekwa katika muda wa matazamio au kituo rekebishi, JOS na taasisi hiyo wataamua iwapo mwanafunzi huyo anaweza kuendelea na masomo yake.
  **KUMBUKA:** Hata kama taasisi hiyo inamruhusu mwanafunzi kuendelea na masomo, hakuna uhakika kama JOS itagharamia mahitaji mengine ya maisha ya mwanafunzi huo.